# *Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo*

## 1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21- 30 SEPTEMBA, 2023 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 01- 10 OKTOBA, 2023

### 1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 21- 30 SEPTEMBA, 2023

Katika dekadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo katika kizio cha Kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kudhoofika wakati ile iliyopo katika kizio cha Kaskazini (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika. Hali hii iliendelea kusababisha ukanda mvua (ITCZ) kusogezwa kuelekea kusini na kuwepo katika maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria na magharibi mwa nchi. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani liliendelea kuwepo katika eneo kubwa la bahari ya Hindi, hali hii ilichangia katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani.

### 1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21-30 SEPTEMBA, 2023

Viashiria vya hali ya hewa tajwa hapo juu kwa pamoja vilipelekea vipindi vichache vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika maeneo ya Ukanda wa ziwa Viktoria na Magharibi mwa nchi na vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache ya Nyanda za juu Kaskazini Mashariki na maeneo ya ukanda wa pwani ya Kaskazini.

## 2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 01-10 OKTOBA, 2023

### 2.1 VIASHIRIA NA MFUMO YA MVUA KWA TAREHE 01-10 OKTOBA, 2023

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo Kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kudhoofika wakati ile iliyopo katika kizio cha Kaskazini (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kuimarika. Hali hii inatarajiwa kuendelea kuimarisha ukanda mvua (ITCZ) kuwepo katika maeneo ya ukanda wa ziwa

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

Victoria na magharibi mwa nchi. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo kubwa la bahari ya Hindi, hali hii inatarajiwa kuendelea kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani.

### 2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 OKTOBA, 2023

**Kanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):** Mvua na ngurumo za radi katika maeneo machache zinatarajiwa.

**Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):** Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla, hata hivyo maeneo machache yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua nyepesi.

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Mvua katika maeneo machache zinatarajiwa.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Mvua na ngurumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Vipindi vya ukavu vinatarajiwa.

**Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):** Vipindi vya ukavu vinatarajiwa.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Vipindi vya ukavu vinatarajiwa.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro):** Vipindi vya ukavu vinatarajiwa.

Imetolewa na;

***MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA***

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz